JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

**23 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**KIKAO CHA THELATHINI NA NNE – TAREHE 23 JUNI, 2015**

**I. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**244. MHESHIMIWA SAID MOHAMED MTANDA (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Tangu mwaka 2010 nimekuwa nikiiomba Serikali kutenga kiasi cha Shilingi 380,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Kijiji cha Mchinga II lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika:-

(a) Je, ujenzi wa daraja hilo utaanza na kukamilika lini;

(b) Je, ujenzi huo utakapokamilika Serikali itakuwa tayari kulifungua daraja hilo rasmi.

**245. MHESHIMIWA FAITH MOHAMED MITAMBO (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mwaka 2010 Mhe. Rais alitoa ahadi ya kumaliza tatizo sugu la maji Mjini Liwale na kwenye Kijiji cha Kichonda:-

Je, mpango wa kumaliza tatizo hilo la maji Liwale Mjini na kwenye Kijiji cha Kichonda limefikia hatua gani.

**246. MHESHIMIWA YUSUPH ABDALLAH NASSIR (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Miradi ya Miji Mkakati (*Strategic Cities*) imekumbwa na urasimu mkubwa sana katika utoaji wa fedha zake hasa Korogwe mjini;

(a) Je, ni kwa nini Serikali haitoi pesa zote kwa mkupuo ili mradi wa stendi mpya (*Bus Stand*), soko jipya na kilomita mbili na nusu (2.5 km) za lami zijengwe kwa wakati mmoja;

(b) Je, ni kigezo gani kimetumiwa na Serikali (Hazina/TAMISEMI) kuzizuia fedha hizi na kuzuia kwa makusudi maendeleo ya Wananchi wa Korogwe hasa ikizingatiwa kuwa fedha hizi ni za wafadhili;

(c) Leo ni miaka miwili na nusu tangu kuwe na ucheleweshaji huu wa makusudi; Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kutoa fedha zote za miradi yote tajwa hapo juu.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**247. MHESHIMIWA CHRISTOWAJA GERSON MTINDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Hapa nchini kumekuwepo na utoroshaji wa wanyamapori hai wakiwemo Twiga kwenda Uarabuni:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukomesha uharamia huo ili kulinda utalii wetu.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**248. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Baadhi ya majengo ya Hospitali ya Jeshi ya Lugalo yamechakaa na baadhi ya vitendea kazi pia vimechakaa:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha ili kukarabati majengo na kupata vifaa vipya vya kutendea kazi.

**WIZARA YA MAJI:**

**249. MHESHIMIWA SALVATORY NALUYAGA MACHEMULI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria uliofadhiliwa na World Bank na ADB wenye chanzo chake kijijini Chabilungo umesimama kwa muda sasa:-

Je, ni nini tatizo la kusimama kwa mradi huo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**250. MHESHIMIWA DAVID ZACHARIA KAFULILA (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wakati Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mhe. Hadija Nyembo akihutubia Kijiji cha Karago Wilayani Uvinza alisema, Wabembe wote wanatikiwa warudi DRC:-

Je, ni nini msimamo wa Serikali kuhusu jambo hili na hatma ya Uraia wa Jamii za Wabembe ambao ni zaidi ya robo ya wakazi wa Wilaya ya Uvinza.

**251. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na udhaifu mkubwa wa vyombo vya dola katika kufuatilia kesi za watoto wanaofanyiwa vitendo viovu kama kubakwa, kulawitiwa, kuchomwa moto na ukatili wa aina nyingi; na kwa sababu njia ya kutoa semina kwa wanaoshughulikia masuala haya haijasaidia kitu:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwepo Mahakama maalum ya kushughulikia masuala ya watoto;

(b) Vituo vya Polisi mara nyingi vimekuwa vikifumbia macho vitendo viovu na madhara yanayowapata watoto kwa kuwalinda watuhumiwa pale wanapopelekewa taarifa za matukio hayo; Je, Serikali inachukua hatua gani kuondoa tatizo hilo;

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kumaliza na kukomesha uovu huu dhidi ya watoto.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**252. MHESHIMIWA MARYAM REUBEN KASEMBE (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Jimboni Masasi, aliagiza kuwa vijiji vyote ambavyo vilirukwa kupatiwa umeme katika Barabara Kuu itokayo Mtwara – Mkarakate vipatiwe umeme:-

Je, ni lini vijiji hivyo ambavyo orodha yake iko **TANESCO** vitapatiwa umeme.

**253. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kuna maradi uliobuniwa miaka mingi iliyopita wa kupata umeme wa maji Kutoka Mto Ngono ambao ulisimamiwa na Mashirika ya dini Bukoba; Maandiko ya mradi yalishafanyika na ilionekana umeme wa megawati 14 unaweza kupatikana:-

Je, Serikali ina mapango gani wa kuendeleza mradi huo.

## WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

### 254. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Ukuaji wa Kilimo ni muhimu katika kuinua uchumi wa Wananchi na pato la Taifa; hata hivyo katika mwaka 2013 kilimo kilikuwa kwa asilimia 4.3 (4.3%) kama ilivyokuwa kwa mwaka 2012:-

Je, baada ya kuanzisha programu ya matokeo makubwa sasa (BRN) kuna mabadiliko yoyote katika Sekta ya Kilimo.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

## WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

## WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

*(Majadiliano yanaendelea)*

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa kwa Hatua zake zote)***

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha matumizi ya Serikali wa Mwaka, 2015 *[The Appropriation Bill, 2015]*

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**23 JUNI, 2015** **KATIBU WA BUNGE**